



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ZOEZI LA KUPITIA NA KUFANYA
UAMUZI WA RUFEEA ZA WAGOMBEA UBUNGE

Dar es Salaam, 09 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 08 Septemba 2020 imeendelea na zoezi la kupitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi rufaa za wagombea Ubunge zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa Wasimamizi wa Uchaguzi nchi nzima.

Rufaa hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 40(6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa Ubunge kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Katika kikao hicho, Tume ilizipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi rufaa **34** kama ifuatavyo:-

- i. Imekubali rufaa **11** na kuwarejesha wagombea husika katika orodha ya wagombea. Rufaa hizo ni kutoka kwenye majimbo ya Ilemela, Tunduma, Kigamboni, Igalula, Madaba, Singida Magharibi (**rufaa tatu**) na Bagamoyo (**rufaa tatu**).

- ii. Imekataa rufaa 8 za wagombea ambao hawakuteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye majimbo ya Singida Magharibi, Bahi, Handeni Vijijini, Madaba, Singida Mashariki (**rufaa mbili**) na Ileje.
- iii. Imekataa rufaa 15 za kupinga walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye majimbo ya Mwanga, Mafinga Mjini, Meatu, Kisesa, Manonga, Igunga na Ilala (**rufaa tisa**).

Idadi hii inafanya jumla ya rufaa za wagombea Ubunge zilizofanyiwa uamuzi na Tume kufikia 89, hii inafuatia taarifa kwa umma iliyotolewa jana tarehe 08 Septemba 2020, ambapo Tume ilitangaza uamuzi wa rufaa 55. Tume itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufaa hizo kila siku. Wahusika wa rufaa hizo wameanza kujulishwa kwa barua juu ya uamuzi wa Tume.


Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI